

HALMASHAURI YA MJI WA KASULU



21/10/2022

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kasulu anapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa ametoa fedha kiasi cha Tshs. **84,000,000/=** kwa ajili ya **Ujenzi wa Shedi mbili katika soko la mazao mnadani.**

Tunakaribisha wazabuni wote wenye mikataba na GPSA ya mwaka 2022-2023 kufika ofisi ya katibu wa bodi ya zabuni kuchukua fomu za mahitaji ya vifaa mbalimbali vitakavyo tumika kwenye muradi huo ili wajaze bei ya kila bidhaa kwa kupata ushindani zaidi wa bei.

Mafundi wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi zote katika fani za uashi, useremala, kupaua na blandering, umeme wanashauriwa kuomba kazi za ufundi. Kwa ajili ya kuepuka ucheleweshaji, unapoomba kazi unashauriwa iwe karibu na makazi yako.

Mafundi wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

A: FUNDI UASHI.

- 1). Awe na uwezo wa kujenga shedi pamoja na kunyanya jengo , kupiga lipu , kuweka vigae na kupaka rangi.
- 2) .Awe ameshawahi kufanya kazi inayofanana na kazi hiyo yenye thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua Tshs. **2,000,000.00**.
- 3) .Awe na uwezo wa kusoma michoro na kufanya makadirio ya mahitaji.
- 4).Awe na uwezo wa kuweka sakafu za aina mbalimbali (kawaida, tiles na terrazo).

B: FUNDI SEREMALA:

- 1). Awe na uwezo wa kutengeneza meza za kufanya biashara.
- 2).Awe ameshawahi kufanya kazi inayofanana na kazi hiyo yenye thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua Tshs. **1,000,000.00**.

3). Awe na uwezo wa kusoma michoro na kufanya makadirio ya mahitaji.

C: FUNDI WA KUPAUA:

1). Awe na uwezo wa kuezeka na kupiga blundering.

2). Awe ameshawahi kufanya kazi inayofanana na kazi hiyo yenyeye thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua Tshs. **1,000,000.00**.

3). Awe na uwezo wa kusoma michoro na kufanya makadirio ya mahitaji.

4). Awe na uzoefu wa kuezeka vizuri majengo.

D: FUNDI UMEME:

1). Awe na uwezo wa kuandaa na kuweka mfumo wa umeme.

2). Awe ameshawahi kufanya kazi inayofanana na kazi hiyo yenyeye thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua **Tshs. 500,000.00**.

3). Awe na uwezo wa kusoma michoro na kufanya makadirio ya mahitaji.

4). Awe na uzoefu wa kufunga mifumo ya umeme katika majengo ya serikali.

MASHARTI YA UJUMLA KWA WAOMBAJI

1. Mwombaji Lazima awe Raia wa Tanzania mwenye Umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea,

2. **Kwa fundi aliyekwisha fanya kazi ya ujenzi kwenye majengo ya Serikali, nakala za barua ya kutunukiwa kazi ni moja ya kigezo cha kupata kazi hii;**

3. Mwombaji lazima awe na namba ya utambulisho ya Mlipa kodi (TIN Number)

4. Mwombaji lazima awe na akaunti ya Benki iliyo-hai,


5. Mwombaji lazima aandike barua ya maombi akiwa ameambatanisha nyaraka zote kama ziliviotajwa katika tangazo hili,

6. Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya Fax, Telefax, Telegraphic system na posta hayatapokelewa,

7. Mwombaji awe tayari kufanya kazi kwa awamu na siku za mwisho wa wiki itakapolazimika kufanya hivyo,

8. Mwombaji awe na timu ya kutosha ya mafundi wasaidizi na vibarua wenyewe weledi na kazi.

9. Fomu za mchanganuo wa kazi za ujenzi zinapatikana katika **OFISI ZA MUHANDISI WA HALMASHAURI YA MJI KASULU** kuanzia saa 1.30 asubuhi Mpaka saa 9.30 alasiri,
10. Fundi atahesabika kuwa ameshinda baada ya kusailiwa ufundi wake kwa **maswali/vitendo (technical evaluation)** na **gharama za ufundi (financial evaluation)**,
11. **Fundi lazima ajaze vipengele vyote vilivyoainishwa katika fomu ya mchanganuo wa gharama za ujenzi,**
12. Barua za maombi zote ziwasilishwe kwa njia ya mkono **Ofisi ya Mkuu wa kitengo cha Ugavi na manunuvi.**
13. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni **Tarehe 28/10/2022 saa 4:00 asubuhi.**
14. Utataarifiwa siku ya Usaili, hivyo namba yako ya simu ni muhimu.


**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI
KASULU**
UTAWALA
HALMASHAURI MJI KASULU.